Title: MOTHER'S DAY
Preached by Dr. w euGENE SCOTT, PhD., Stanford University
At the Los Angeles University Cathedral
Copyright © 2007, Pastor Melissa Scott. - all rights reserved

Somo: SIKU YA KINA MAMA
Imehubiriwa na Dk. w euGENE SCOTT, Shahada ya Falsafa., Chuo Kikuu Cha Stanford
Katika Kanisa Kuu la Chuo Kikuu, Los Angeles
Haki © 2007, Mchungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa

# SIKU YA KINA MAMA

Nimekuwa sio mwaminifu kwenye kanisa hili kuu kama nilivyokuwa sehemu nyingine kuhubiri ujumbe ambao nahubiri kila mwaka. Mwaka huu ninarudi kwenye ule mfano. Na ni siku ya kina mama, kwa hiyo narudi kwenye ujumbe wa kila mwaka ambao ninao katika kijitabu changu kidogo. Somo ni *Mungu hakuweza kuwa kila sehemu?… Kwa Hiyo Aliwaumba wakina Mama!* Nafikiri kuna kitu kimoja katika kifaa cha kamera pale ikiwa kamera inataka kukiokota mahali fulani.

“Mungu hakuweza kuwa kila mahali, hivyo aliwaumba wakina mama!” Ni methali ya kale ya kiyahudi. Ninaweka alama ya kuuliza mbele yake kwenye kichwa cha somo kwa sababu sisi tunajua, tunapofikiri kuhusu jambo hili, kwamba Mungu anaweza kuwa kila mahali. Haya ni mafundisho ya kuwa Mungu yuko kila mahali. Na ninamuona mtu aliyerudia kuandika tena aliamua kubadilisha alama yangu ya kuuliza na kuwa alama ya mshangao ili kwamba ionekane iko sawa, lakini ni mawazo mazuri na ya ajabu. “Mungu hakuweza kuwa kila mahali, hivyo aliwaumba wakina mama,” na labda alama ya mshangao ni sahihi kwa sababu Mungu anaweza kuwa kila mahali kwa kufanya kazi na kina mama kwa kutumia roho yake. Katika kitabu hiki ninazo sentensi kuhusu wakina mama. Nitaenda kuzisoma tena—yawezekana zitakuwa mpya kwa wengi wenu ambao mmekuja kwenye familia ya nyumba ya mfalme tangu nilipohubiri hivi huko nyuma.

“Katika siku ya hukumu, Malaika anayetunza kumbukumbu
atawasamehe sana ambao
wanaweza kusema, ‘Sijawahi kumfahamu mama yangu.’”

—Charles Lamb

“Hivi vyote jinsi nilivyo, ni mama yangu amefanya.”

—John Quincy Adams

“Vita hodari vilivyowahi kupiganwa;
Niwaambie ni wapi na lini?
Kwenye ramani ya duniani hutapaona mahali hapo,
Vilipiganwa na wakina mama wa wanaume.”

—Juaquin Miller

“Mama ni mama mkimya
kitu kitakatifu kiishicho.”
—Coleridge

“Wanaume wako hivyo kwa sababu mama zao wamewafanya hivyo.”

—Emerson

“Kwa askari aliyeanguka kwenye uwanja wa vita,
tunakupa kinyago na kibao.
Lakini kwa mama, ni vita
bila utukufu.
Havai medali za taifa.
Beji yake ni mistari yenye mashimo
Kwenye uso wake.”
—Asiyejulikana

“Miaka kwa mama huleta shida,
lakini haifanyi upendo wake kuwa mdogo.”
—Woodsworth

“Amebarikiwa alivyo, Mungu alimuumba hivyo,
Na matendo ya kila wiki ya utukufu
Yanaanguka kwa ukimya kama theruji.”
—Lowell

Baadhi katika siku ya kina mama wanavaa nguo za rangi ya ua kuashiria kwamba mama yao amekwenda. Mwingine aliyekutana na uzoefu huo, na akamkumbuka mama, aliandika mistari hii:

“Wakati wote aliegemea kutuangalia sisi,
Kwa wasiwasi tulipokuwa tumechelewa,
Wakati wa baridi alikuwa dirishani,
Wakati wa kiangazi alikuwa langoni.
Mawazo yake yalikuwa yamejaa sisi—
Hakuweza kusahau!
Na lazima alikuwa bado akitazama.
Akisubiri mpaka tunapokuja kwake,
Kwa wasiwasi tulipokuwa tumechelewa—
Akitazama kutoka kwenye dirisha la mbinguni,
Akiegemea lango la mbinguni.”
—Margaret Widdemer

Na nimeshasema hilo, wayahudi wana msemo katika methali zao: “Mungu hakuweza kuwa kila mahali, hivyo aliwaumba wakina mama.” Lakini kama alichukua hatua moja zaidi, Mungu ambaye ni kila kitu anaweza kuwa mama pia.

Mwanzo 17:1: “Bwana, akamwambia Abramu, Mimi ni Mungu mwenyezi.” *El Shaddai*: jina hili linatokana na neno Shad ‘matiti ya mama.’ Hivyo *El Shaddai* ni ‘anyonyeshwae’ na inatokana na hiyo

maana ya mama anayemnyonyesha mtoto wake mdogo asiye na msaada kwenye matiti yake, kwa hiyo inaashiria kwamba yeye ni mtoa nguvu, anayerutubisha. Ni mojawapo ya picha chache kwenye maandiko ambapo Yeye Mungu anajilinganisha na kazi za mama anaposema, "Mimi ni *El Shaddai*." Ethel Clemance atamkumbuka baba yake Dk. Price ambaye alikuwa akitafsiri hilo jina kwa tafsiri ambayo ina maana 'Mungu atoshaye.' Mungu anayetosha. Chochote unachohitaji, Yeye anatosha. Kadhalika mama anayemshika na kutunza mtoto katika matiti yake na kumpa kila kinachotakiwa kwa ajili ya nguvu ya yule mtoto na virutubisho vinaonyesha ule mtazamo wa Mungu, lakini Mungu zaidi anaelekeza katika Isaya 66. Hapo anasema katika ile Biblia ya tafsiri ya *King James*, "mfano wa mtu ambaye mama yake amfariji," (Isaya 66:13), "Kama mama yake amfariji, ndivyo nitavyowafariji ninyi."

Sasa ujumbe wa leo umewafikia pale mlipo. Huu sio ujumbe ambao tutaenda kufungua maandiko ya kweli, unabii ambao unatupa uelewa wa mkono wa Mungu katika historia. Sio majadiliano ya kitheologia ambayo tumekuwa nayo hapo nyuma, ambayo ni mara mbili—angalau katika sehemu hizi mbili, Mungu anaruhusu suala au mtazamo wa kazi ya mama hapa duniani inapatikana katika ufunuo wa kwamba anatupa sisi kile ambacho atakuwa kwa watu wake; na, "Kama mama anavyofariji, hivyo nitawafariji ninyi," Mungu mwenyewe ajidhihirishe kwa kile ambacho tunachoweza kukipokea kuhusu kazi ya mama duniani.

Sasa Yesu alitumia ishara ya baba alipoongelea kuhusu "Baba yetu wa mbinguni**"**, Aleta jambo la kufananisha na anasema, kama ukienda kwa baba yako wa duniani na ukimuomba mkate, hatakupa jiwe; kama ukienda kwa baba yako wa duniani na kumuomba samaki, hatakupa nyoka. Vivyo hivyo, anaruka—baba yetu wa mbinguni anapenda kutenda mambo mazuri kwa ajili yako. Kama Yesu, akielekeza kwa vile tunavyojua—angeweza kuiinua na kusema chochote anachoweza kupokea kwa yale maelezo ya kidunia, baba yetu wa mbinguni ni zaidi…, na hii ndio leseni yangu katika hiki kuangalia kina mama wa duniani katika mtazamo wao wa kufariji na kupenda kwa sababu siku hii inatupa ule mwelekeo mzuri na kumbukumbu ya jinsi wakina mama walivyo na maana kwa kile wanachokifanya.

Naweza kumtazama mama wa hapa duniani katika maandiko. Angalia upendo wake, na usema katika msingi, "Kama vile yule mama yake anavyomfariji, ndivyo nitakavyowafariji ninyi" ni kiasi gani leo na siku nyingine, tunaweza kumuangalia mama yetu wa mbinguni, ambaye ni *El Shaddai* inatupa leseni ya kusema, "kama tukiona upendo kutoka kwa mama yetu wa duniani, si zaidi na ni kiasi gani mama yetu wa mbinguni anavyotufariji." Ni mbaya sana kwa wanawake wote, wapo hapa leo. Waambie kuhusu hili. Hawataamini kwamba nilihubiri ujumbe huu.

Nitaangalia wakina mama watatu kwenye Biblia:

Yokebedi. Lazima twende mbele kidogo kwenye kitabu cha Kutoka 6 kupata jina la mama yake Musa. Na atatupa mtazamo mahususi unaoangalia suala fulani, mtazamo wa upendo wa mama ambao ukionekana unaweza kusema, "Ni kiasi gani baba yetu wa mbinguni." Nyote mnajua hiyo hadithi. Miaka 400 ilikuwa inakaribia wakati Mungu alipomuahidi Abramu watu wake wangepelekwa…, wao wake, ambao, wangepelekwa kwenye vifungo na kuangukia kwenye utumwa; na wangekombolewa na kurudi kwenye sehemu ya ahadi aliyopewa Abramu. Farao, alijua kuhusu huo utabiri. Alijua muda ulikuwa umeshapita na aliendelea kumaliza watoto wote wa kiume waliozaliwa na watumwa ili kuondoa uwezekano wa mkombozi kukua—watoto wote wa kuime walitupwa kwenye mto wa Naili.

Yokebedi—jina la kwanza kwenye maandiko linalohusishwa na Yehova. Ni neno moja (lenye muunganiko wa maneno mawili) ambalo linalohusiana na jina lake Yehova. Kwa kweli ina maana "utukufu wa Yehova." Yokebedi ni mjamzito, na mtoto anapokuwa ndani ya tumbo lake, akiishi kwenye kibanda cha motope na nyasi, cha kitumwa, hofu lazima ilikuwa ikimpata—"atakuwa ni

mvulana au msichana?" …katika maarifa kwamba ni mvulana, atauliwa mara moja na kutupwa kwenye mto—kuuwawa. Hakika wakati mtoto anapozaliwa ni mvulana.

Sasa nataka uone jinsi Yokebedi anavyoonyesha upendo wa mama, kwa wasio na tumaini na msaada, wale ambao wamekumbwa na hali hii—kwa mfano huu, sio wa Musa kuchagua; …wale ambao wamepatwa na hali ngumu ambazo ni zaidi ya uwezo au nguvu zao, ambao wanazungukwa na hali ya kutokuwa na msaada na matumaini, na hapa inaongelea kitu kimoja tu: maanzamizo yako, kushindwa kwako, mwisho wako. Ninaona huyu mama Yokebedi na mtoto nuyu ambaye kila kilio chake kilileta tishio kwa askari walioteremka. Angalia huyu mama aliyekuwa mtumwa bila haki ya aina yoyote. Kwa miezi mitatu mizima aliweza kumficha mtoto wake—kwa jinsi fulani anazuia kilio chake kisisikike kwa miezi mitatu mizima.

Hivi leo hapa wapo wakina mama ambao wanajua adha ya miezi mitatu ya mwanzo ya kulea mtoto. Kila saa, kila siku: "atagundulika?" Na anaweza kufanya kitu chochote; Musa hawezi kufanya kitu chochote.

Anabuni njia. Kwa jinsi fulani au nyingine anafanikiwa kuleta majani na matope kutoka kando ya mto na kutengeneza kikapu kidogo. Kwa jinsi fulani anafanikiwa kupata wapi binti mfalme anapokwenda kuoga kila siku. Nina hakika kwamba si kitu fulani cha maarifa ya kawaida kati ya watumwa. Kwa jinsi fulani anafanikiwa kukatiza kwenye mitaa ya ule mji wa watumwa kule Memphis akimbeba mtoto, akijua kwamba kwa muda wowote atagundulika, tumeshasema atachinjwa. Kwa jinsi fulani aliweza kumuweka katika kikapu kidogo kilichotengenezwa kwa majani kwenye sehemu ile ile ambayo angeweza kuogelea juu ya maji ili aonekane na binti mfalme wa Misri.

Na kwa jinsi fulani au nyingine anafanikiwa kumpata binti yake Miriamu amefichwa ili binti mfalme atakapomgungua Musa…. Na hakika, kwa sababu alikuwa ni …, kama maandiko yanavyosema, "mtoto mzuri", binti mfalme anataka kumtunza; na mara Miriamu anajitokeza mbele—kwa sababu binti mfalme alimtambua kuwa ni mtoto wa Kiebrania, na anasema, "tungependa mama wa Kiebrania amtunze mtoto?" Na hakika unafahamu—mwisho wa hadithi yote—anatunzwa kama mwana wa mfalme katika nyumba ya Farao, na kwa uamuzi wake mwenyewe atawaongoza wao kutoka kama mkombozi wao.

Sasa kila mmoja wa hawa wakina mama atauzingatia ujumbe huu kwa jinsi ambayo sio kila mtu atakavyouona kuwa unafaa. Sehemu hii ya ujumbe ni kwa wale—ni hakika wako katika kundi dogo la huu mkutano, wale ambao wako katika hofu ya hali ambazo zinakufanya ukose msaada na matumaini. Hakika kuna baadhi watakuwa wanasikiliza kupitia runinga. Huu ujumbe uko wazi; huyu mama wa hapa duniani anaashiria kile kila mama anachokijua kuhusu upendo wa mama usioisha: Hatashindwa kukabiliana na hizo hali; hatakubali kushindwa; atatafuta njia, haijalishi kitu gani kitakachomgharimu kumkomboa huyu mtoto asiye na msaada kutoka kwenye hali isiyo na njia. Lakini anaipata njia kwa kutumia mali zake chache alizonazo, ingawa alikuwa mjakazi mtumwa. Alipata upendo usioisha, usiokata tamaa kwa wasio na msaada, alipata njia.

Ruka: Mama yetu wa mbinguni—kutumia neno hili bila kuomba msamaha au maelezo mengine, Mama yetu wa mbinguni, si kama Yohebedi, pia ni Bwana wa majeshi. Hana mipaka katika uweza wake. Ana uumbaji wote katika mikono yake.

Yote Yokebedi anayoniambia mimi ni kwamba kwenye moyo wa Mungu ambao umemfanya yeye mwenyewe ajidhihirishe katika Isaya 66, "Kama mama anavyofariji, ndivyo nitavyowafariji ninyi," …katika moyo ule Mungu ni ule ule upendo, "kama mama wa kidunia hatakata tamaa na hatasema ufe na hataacha kukutunza mpaka apate njia ya kumkomboa mtoto asiye na msaada, si zaidi jinsi Baba yetu wa mbinguni atakavyowakomboa ninyi?" Huu ndio msingi wa mstari kwenye maandiko unavyosema,

"Hatakujaribu kupita kiasi cha uwezo wako." Huu ndio msingi wa mstari kwenye maandiko unavyosema, "Sitakuacha na wala sitakupungukia." Na tuiangalia mistari hii yote tena. Huyu ni Mungu, Mama yetu wa mbinguni katika upendo wake kwa wasio na msaada. Unaweza kukosa msaada; Mama yetu wa mbinguni ni mwenye nguvu na msaada. Hatakata tamaa, hatakuacha bila msaada.

Mama wa pili. Ninataka umwangalie katika nuru ya tofauti kwa sababu amekuwa akitukuzwa sana, amkuzwa sana, amafanywa kuwa mtakatifu, ambaye ni mama wa duniani, upande wake ambao ni upande wa kweli, unakosekana. Yohana 19, mstari 25: Mary (*Mariamu)*—jina maarufu duniani. Kwa mara ya mwisho nilifanya utafiti, ulikuwa ni muda wa nyuma kidogo—mwaka 1957: kulikuwa na wanawake 3,720,000 walioitwa Mary (*Mariamu)*—katika nchi hii. Haijalishi ni wapi unaelekea, anapendwa dunia nzima.

Katika kitabu hiki, naongelea kuhusu safari ya Tahiti—nje kidogo ya kanisa katika kisiwa cha kaskazini. Mtazamo: Mary *(Mariamu).* Juu na kando ya uwanda wa La Paz, Bolivia—sehemu pekee duniani ambapo ndege zinaruka mpaka kwenye ardhi, uwanja wa ndege mrefu kuliko viwanja vyote vya ndege duniani. Kama ukiacha uwanja wa ndege na kuona uwanda wa juu wa Andes kwa mbali, ghafla unafika kwenye ukanda wa milima na barabara inajikunja kwa chini kuelekea La Paz ambayo ipo chini ya bonde. Tunakuja kwenye barabara chakavu ilibidi tusimame na kupumzika. Kundi kubwa lilikuwa limebeba picha ya Mary *(Mariamu)* na kitu kama mshale ukiwa unauchoma moyo wake, msemo ulioshauriwa na Simon; aliinuliwa na Wakatoliki kuwa mtakatifu.

Waliukuza wajibu wa mama, kama vile utakavyoelezwa ukubalike na Kristo, kwa sababu walishasahau kwamba Mungu hakumuhitaji Mariamu kuwa mama. Yeye mwenyewe alikuwa na sifa hizo za mama.

Nataka umwangalie Mariamu, sio kama mtakatifu bali mwanadamu wa kawaida. Nataka umwangalie yeye kama Agano Jipya linavyomdhihirisha: yeye ambaye hakumuelewa mwana wake; yeye ambaye alimtazama kwa mtazamo wa kibinadamu, bila kujali unabii uliotolewa, alimuona kwa kutumia macho yake ya kimwili. Nataka umwangalie yeye kutoka ndani ya hisia zake za kiuanadamu za kukataliwa, asiyemuelewa kabisa mtoto wake, kuangalia hofu zake alitambua alipokuwa ameangikwa msalabani huku damu ikimtoka na alikufa msalabani. Bado Yohana 19:25 inasema, "Na penye msalaba wake alikuwa amesimama mamaye… penye msalaba alikuwa amesimama …na penye msalaba wake alikuwa amesimama mamaye"—na hii inaashiria upendo kwa mtu aliyekataliwa.

Kama Musa katika ujumbe huu anaonekana katika kazi yake ya mwanzo kama mtu asiye na msaada—wote wasio na msaada wanaweza kutambulika; Yesu katika mwili huu na katika wakati huu, anaoneakana kwa kupitia upande wa mama wa kidunia (kuliko ule unaoeleweka wa kimungu-kinabii), alikataliwa na watu, ukinukuu Isaya: "Alikuja kwa ajili yao na hawakumpokea."

Alimtazama akiongozwa mitaani, akipiga kelele, akigombana, alikiwa amebeba msalaba. Alisimama na akamtazama mwanaye kama mtoto mikononi mwake. Zaidi ya hayo yote anaweza kutufundisha, hakuonekana na kiasi cha uelewa ambao haukuwa wake; aliheshimiwa zaidi ya wanawake wote kwa kumbeba tumboni mwake mwana wa Mungu. Kwake yeye, Yesu alikuwa mtoto. Unaweza kuona kuchanganyikiwa kwake wakati mtoto wake alipokuwa na miaka 12, alipopotea, aliondoka Yerusalemu, akilia, "Baba yangu na mimi walikuwa wakikutafuta—baba yako na mimi." Alimkemea, tena nina hakika ni kwa sentensi ya aina ya pekee: "Lazima niwe karibu na mambo ya Baba yangu," akimaanisha Baba yake wa mbinguni.

Nyuma kidogo kabla ya kuandika hiki kitabu, nilikaa usiku kwenye mwanga wa mwezi juu ya Mlima Tabo kule Israeli, kwa muda wa saa moja nikiangalia taa za Nazareti na vilima vidogo vilivyoinuka

ambavyo vinaonyesha muonekano fulani, na kuonyesha matukio pale Nazareti ambapo Yesu alipoanzia kuhubiri. Na familia—ikionyesha uchungu wa raia wake wa mji huu kwa madai kwamba Yesu alikuwa akijifanyia mambo yake mwenyewe na walisikika wakisema kwa dhihaka, "Huyu siye mwana wa selemara?"— …alikuja kumuokoa yeye kutoka kwa walichokijua kuwa ni kundi la watu wabaya ambao walitaka kumkataza yeye kusema mambo ambayo yeye akitaka kusema. Alikemewa, kama Yesu alivyowatazama waliposema, "Mama yako na ndugu zako wanakutafuta," na alisema, "Mama yako ni nani? Nani ni ndugu yako? Ni wale wanaofanya mapenzi ya Baba aliyenituma mimi. Hawa ndiyo ndugu zangu."

Bado haijaeleweka katika kifungu hiki, ninarudia, mama yake alimuona alitoka damu, akifa na kukataliwa na watu wote, hakuzimia moyo, hakukimbia, hakuanguka. Alisimama kando ya msalaba wake wakati uhai wake ukimtoka. Upendo kwa aliyekataliwa.

Nina hakika kabisa ya kuwa hajawahi kuwapo mtu yeyote kwenye uso wa dunia hii ambaye kwa sababu sisizo za msingi alikataliwa kama Yesu wa Nazareti alivyofanyiwa. Hapa sielezei msalaba mbele yetu katika maana ya kithiologia; ninauelezea msalaba kwa uelewa mdogo wa mama yake, kwa mtazamo wa kidunia. Kwake yeye, mwanaye anaangikwa msalabani katikati ya wezi wawili—kama kitu kisichovutia, kisichopendwa, kilichokataliwa. Hakumkataa. Upendo wake haukupungua. Alisimama—Nina hakika kila mama anajua jinsi uchungu ulivyo—wa pili tu kutoka kwa Yesu mwenyewe au Baba wa mbinguni mwenyewe alimuona mtoto wake akiteswa. Kwa hakika alikaa mstari wa tatu, lakini akisimama pale. Asingemkataa yeye ingawa dunia nzima ilimkataa yeye.

Kama Yokebedi anaweza kukupa faraja—"Kama mama anavyofariji ndivyo nitakavyowafariji ninyi,"—kama Yokebedi anavyokufariji haijilishi kwa kiasi gani hali yako au yangu ni ya kukatisha tamaa, mama yetu wa mbinguni atafanya njia na tutapumzika katika mikono yake. Kama ukiwa mmoja wa wanaoangalia runinga, wanaosikiliza radio, au hapa leo wanaohisi wamekataliwa na kila mtu, mama yetu wa mbinguni anatutegemeza na hatataka tamaa. "Anayekuja kwangu"; mstari huu una maana, "Anayekuja kwangu sitamtupa nje." Huyo ni mama yetu wa mbinguni—usihofu atatutunza kama watu wengine duniani. Upendo kwa waliokataliwa.

Nakwenda kwenye Kitabu cha Samweli wa II Sura ya 21 kuangalia picha ya mama wa tatu. Jina lake ni: Rispa.

Samweli wa II Sura ya 21. Alikuwa ni rafiki wa kike wa Sauli, sio mke wake—suria, lakini alimzalia watoto wa kiume wawili. Sauli, Mbenjamini, alikuwa mfalme wa kwanza aliyepakwa mafuta na Samweli kwa ajili ya kuiongoza Israeli. Katika mwanzo wake Mungu alimpa moyo mpya na alikuwa mfalme mkubwa, lakini nguvu zake zilipoongezeka akabadilika, mpaka mwisho wa maisha yake uliishia kujiuwa na mwili wake ukapigiliwa misumali ukutani na maadui zake karibu na mlima wa Gibeoni; akiandika maandishi kwenye kaburi lake kabla ya kufa, "Nimefanya upumbavu."

Kati ya mambo mengine ya kipumbavu aliyoyafanya ilikuwa kuvunja kiapo alichoapishwa na Yoshua katika siku za mwanzo wakati waisraeli walipokuwa wakienda kwenye Nchi ya Ahadi na Yoshua, akiapa kiapo kwa wagibeoni kwamba Israeli kamwe haitawaangamiza kwa upanga. Sauli, kwa upumbavu, alivunja kiapo. Aliwafukuza wagibeoni; alipanga kuwaangamiza, kuwauwa kwa upanga.

Baada ya Sauli kujiuwa, Daudi alipakwa mafuta kuwa mfalme, wagibeoni walienda kwa Daudi kutaka ushauri kwa sababu Mungu aliwaadhibu waisraeli kwa kitendo cha Sauli kuleta baa la njaa kwenye nchi hiyo. Baa la njaa liliikumba nchi. Na katika kumlilia Mungu kwa kosa hilo…, Daudi alimuuliza Mungu, na Mungu akamwamba ni kwa sababu Sauli amevunja kiapo. Kwa hiyo aliwaomba wagibeoni

wasubiri na akawambia wafanye siku ya utakaso kwa kile Sauli aichokifanya, kuliweka taifa lote kwenye upanga.

Ilikuwa siku mbaya  na katika mfumo wa siku mbaya, iliyo ya kikatili, walisema wanataka wana saba wa kiume wa Sauli—ambao pia waliwapo wale wana wawili waliozaliwa na suria lake Rispa. Waliwataka hao wana saba ili wawanyonge kwenye mlima Gibeoni.  Daudi aliwatoa hao wana saba, waliwanyonga wale wana saba kwenye mlima Gibeoni. Na katika kile kipindi walichonyongwa, Biblia inasema ulikuwa mwezi wa mavuno ya shairi, mwezi wa nne.  Kuanzia mwezi wa nne mpaka mvua zinaponyesha mwezi wa kumi, wale wana walikuwa wakining'inia katika ule mlima. Wagibeoni waliazimia kuwanyonga daima.

Sasa, mama wa hawa wana, Rispa, alipokwishajua mahali ambapo wana wale waliponyongwa, pamoja na wanae, alikwenda kwenye mlima wakati ule ule, na akasema, mavuno ya shayiri ni mwezi wa nne, akibeba nguo za magunia kwa ajili ya kuomboleza au kukalia au kufanyia hema dogo. Usiku na mchana kutoka katika mavuno ya shayiri mpaka kunyesha kwa mvua mwezi wa kumi, Biblia inasema alikaa kwenye mlima huo. Aliwafukuza ndege mchana; na usiku alifukuza wanyama.  Mwezi wa nne…, mwezi wa tano …, mwezi wa sita …, mwezi wa saba …, mwezi wa nane …, mwezi wa tisa …, mwezi wa kumi … miezi saba.  Miezi saba mirefu, alikaa kwenye ule mlima. Mchana; usiku. Narudia, akifukuza ndege mchana, na usiku akifukuza wanyama.

Sasa hatari ya kupingwa, hebu nijilazimishe na neno linaloleta picha kwenye mawazo kuchoma kwenye ile miili saba iliyotundikwa pale. Mwili ungeweza kuanza kuoza na kuanguka kutoka kwenye mifupa, jua lingeifanya iwe na weusi, inchi moja baada ya nyingine jinsi miezi ilivyokwenda, wangeanza kusema ….  (harufu mbaya ingezidi.)  Kubaki kwenye ule mlima kwenye miguu ya ile misalaba saba ingekuwa kuendelea kuishi kwenye harufu mbaya na kuendelea kujiweka kwenye mabadiliko kutoka hali nzuri kwenda kwenye hali isiyopendeka na mbaya, kama vipande vya mwili vingeendelea kudondoka kimoja baada ya kingine kutoka kwenye mifupa; na mwili ungeoza na vipande vingedondoka ardhini. Kwa maneno, ninajaribu kulazimisha ili tuweze kuona kitu kinavyokuwa hakipendeki.

Wakati akianza—unaweza kuhisi mwendo na mvuto, hao ndiyo wana wake na wamekufa kwenye mti, lakini kwa woga aliwafukuza ndege na aliwafukuza wanyama, wangebadilika kuwa kitu kisichopendeka, kama nilivyosema.  Haikumdhuru Rispa.  Alikaa pale usiku…, asubuhi…, mchana…, usiku.  Katika kuokoa maisha yake, aliwafukuza ndege, aliwafukuza wanyama.

Hatimaye Daudi—ule moyo mkuu ambao Mungu anamshuhudia kama "Mtu anayeupendeza moyo wake"—hatimaye alisikia habari.  Zilimtisha yeye mwenyewe, alituma neno kuchukua kilichobaki kwenye miili yote; akiunganisha na mifupa ya Yonathani na Sauli; wape sehemu ya heshima ya kuzikia, umrudishe Rispa kutoka kwenye mlima mbaya na umpe heshima anayostahili.

Kama Yokebedi anavyoonyesha ule upande wa Mungu usiokufa, usiokata tamaa, usioachia, usiache mpaka upate njia ya kupata ukombozi wa kukosa kwako msaada; na Mariamu anaashiria ile sifa ya mama wakati wengine wote wakimkataa mtoto wake, anasimama kando yake; Rispa anaashiria ule upendo wa mama wa kuvumilia sana ambao unamfanya awatazame wana wake wakiteketea na kuwa vitu visivyopendeka tena, lakini upendo wake haukuondoka.

Kama mama hawa wa duniani wanaonyesha upendo wa aina hii, je si zaidi siku ya leo tukiwakumbuka mama zetu, tunaweza kutazama nyuma kidogo katika hali zetu za kukata tamaa, kukataliwa, kukosa haki kabisa, na kusema tunamshukuru Mungu kwamba "Kama mama anavyofariji, nami nitawafariji"?

Haijalishi hali yako leo, nina furaha hili kanisa bado lipo kuhubiri upendo wa Mungu badala ya baadhi ya mambo yasiyo na maana ambayo yanafunika ule upande wa Mungu wa asili yake.

Yeye ni Mungu na hajabadilika. Ni *El Shaddai*, mama anayefariji. Ni Mungu, na hatakuacha wala kukupungukia. Jipe moyo katika hali yako: “Kama mama anavyofariji, nami nitawafariji ninyi.”

haki© 2007, Mchungaji Melissa Scott. – Haki zote zimehifadhiwa